




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA
SERIKALI ZA MITAA
WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA
MIJINI-TANZANIA (TARURA)



MRADI SHIRIKISHI WA MAENDELEO YA BARABARA NA UTUMIAJI WA FURSA
ZA KIJAMII NA KIUCHUMI

Mwaliko kwa Umma Kushiriki katika Jukwaa la Mashauriano la Kitaifa
(litakalofanyika Mtandaoni) kutambulisha Mradi pamoja na Nyaraka za Mfumo
wa Kimazingira na Kijamii Zinazohusu Mradi huu

Serikali ya Tanzania, kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na Wakala wa Barabara nchini Tanzania (TANROADS) kwa ufadhili wa Benki ya Dunia, inaandaa Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Barabara katika Utumiaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi (RISE). Lengo la mradi huu ni **"kuboresha upatikanaji wa barabara vijijini na kutoa fursa za ajira kwa wananchi katika maeneo ya vijijini yaliyochaguliwa na kujenga uwezo katika usimamizi endelevu wa barabara za vijijini kwa kujumuisha mbinu za ushirikishwaji wa jamii"**.

Mradi huu utatekelezwa katika maeneo mbalimbali ya barabara za Vijijini katika Mikoa 25 ya Tanzania Bara isipokuwa Mkoa wa Dar-Es-Salaam. Utekelezaji huo utahusisha Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, Kuboresha maeneo korofi au yenye vikwazo mbalimbali, Kufanya matengenezo ya kawaida kwa kutumia nguvukazi (vikundi). Barabara za Mikoa na Vijijini zitakazohusika katika hatua ya awali ni barabara kutoka Halmashauri za Wilaya Sita (6) ambazo ni Wilaya za Handeni Mkoa wa Tanga, Mbogwe Mkoa wa Geita, Ruangwa Mkoa wa Lindi, Mufindi na Kilolo Mkoa wa Iringa. Utekelezaji wa mradi huu katika maeneo mengine ya Tanzania Bara itategemea na upatikaji wa fedha za utekelezaji. Wakati wa Utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Programu ya RISE, TARURA itaandaa Mpango wa Kitaifa wa Barabara za Vijijini, kutekeleza Mpango Mkakati wa kitaifa wa uboreshaji na utunzaji wa barabara za Vijijini, Mpango Mkakati huu utatumika kama mfumo wa uwekezaji wa baadaye katika sekta hiyo kulingana na upatikanaji ya fedha.

Nyaraka zote muhimu za mifumo inayohusu usimamizi wa kimazingira na kijamii zimeshaandaliwa. Nyaraka hizi ni pamoja na: Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii, Mfumo wa Sera ya Uhamishaji mali zinazo athiriwa na mradi, Mpango wa Usimamizi wa Masuala ya Kimazingira na Kijamii, Mpango wa Ushirikishaji wa Wadau, Mfumo unaohusu Taratibu za Usimamizi wa wafanyakazi na Mipango ya Makundi hatarishi.

Jukwaa la Mashauriano Kimkoa tayari limeshafanyika katika Mikoa ya Tanga tarehe 05 Januari 2021, Lindi tarehe 05 Januari 2021 na Geita tarehe 08 Januari 2021.

Kumetokea mabadiliko la Jukwaa la Mashauriano la Kitaifa ambalo lilitakiwa kufanyika tarehe 12 Januari 2021 na sasa litafanyika tarehe 13 Januari 2021 kuanzia saa 3:00 Asubuhi kwa njia ya mtandao, yaani kutumia Programu ya Webinar inayowawezesha wadau kufanya mkutano kwa kutumia intaneti. Ili kuufuatilia Mkutano huo wa Jukwaa la Mashauriano la Kitaifa, Anwani ya

Mtandao (Webinar) itatumwa kwenye Anuani za Barua Pepe za Washiriki pia itapatikana katika Tovuti za TARURA na TANROADS kuanzia tarehe 11 Januari, 2021.

Lengo la mkutano huu ni kuutambulisha Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Barabara na Utumiaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi (RISE) na Nyaraka za Mfumo wa Kimazingira na Kijamii zinazohusu mradi huu kwa umma na wadau wote na kukusanya maoni kwa ajili ya kuuboresha.

Taarifa zote za msingi kuhusu Mpango wa Ushirikishaji wa Maendeleo ya Barabara na Utumiaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi (RISE), Nyaraka zinazohusu Mfumo wa Kimazingira na Kijamii pamoja na Mihutasari yake katika lugha za Kiingereza na Kiswahili zinapatikana katika tovuti zifuatazo za TARURA na TANROADS: tarura.go.tz na tanroads.go.tz. Nakala ngumu za nyaraka hizo zitapatikana katika ofisi zote za Waratibu wa Mikoa na Mameneja wa Halmashauri.

Umma na wadau wote ambao wanatarajia kuwasilisha maoni yao kwa maandishi katika Mradi shirikishi wa Maendeleo ya Barabara na Utumiaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi (RISE) wanaalikwa kufanya hivyo kwa kutumia anwani iliyopo hapa chini:

Mtendaji Mkuu,

Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini,

S.L.P. 11042

TARURA House

Mji wa Serikali, Mtumba

Dodoma, Tanzania

Baruapepe: ceo@tarura.go.tz

Simu: +255745810140